

Vipimo vya kiunzi

Aina ya mzinga	Mchi wa juu(non-spacing)		Mchi wa chini	Mchi wa pembeni
	Upana sm	Urefu sm	Urefu sm	Kimo sm
Langstroth	2.7	48.2	44.8	23.2
Jumbo	2.7	48.2	44.8	28.6
Shallow Dadant	2.7	48.2	44.8	15.9
TCH	3.2	48.2	44.8	23.0

TCH=Tanzania Comercia Hive (Mzinga wa biashara wa Tanzania)

Vipimo vya sehemu ya ndani ya mzinga wa viunzi

Aina ya mzinga	Urefu A (sm)	Upana B(sm)	Kimo C (sm)
Langstroth	46.6	37.7	24.1
Jumbo	46.6	37.7	29.5
Shallow Dadant	46.6	37.7	16.8
TCH	46.6	37.7	24.2

TCH=Tanzania Comercia Hive (Mzinga wa biashara wa Tanzania)

Tanzania Top Bar Hive (TTBH)

Utengenezaji wa TTBH au KTBH lazima uzingatie vipimo thabiti vya mchi. Mchi lazima uwe na upana wa milimita 32 kamili ili kuwezesha nyuki kujenga masega ambayo yatakuwa na mm 32 au 33 kutoka katikati ya sega moja hadi katikati ya sega lingine jirani au linalopakana nalo. Mpangilio huu huacha nafasi ya mm 8 au 9 kati ya nyuso za masega yanayopakana (yaliyokaa sambamba), ili mradi nyuki wawili wanaweza kupishana kwa kugeukiana migongo kwenye nafasi hiyo. Uwezo wa kuzalisha hadi lita 20 za asali (sawa sawa na kilo 30) kwa msimu mmoja; Gharama yake sio kubwa sana.

Sifa za mzinga ya masanduku

- Ni mkubwa kutosheza mahitaji ya kupanuka haraka kiota cha nyuki wa Afrika;
- Uwezo wa kuzalisha hadi lita 20 za asali (sawa sawa na kilo 30) kwa msimu mmoja;
- Umebuniwa kwa kuunganisha sifa za mzinga ya kiasili na mizinga ya mzasanduku ya bara la Ulaya na kuifanya kuwa sahihi sana kwa mfugaji wa kawaida, maana unaruhusu mfugaji kuona maendeleo ya makundi yake. Gharama yake sio kubwa sana




Vipimo Vya TTBH

Michi yote lazima ifungiwe kianzio cha msingi wa sega cha nta kwenye msitari wa katikati.

Vipimo vya ndani vya TTBH (Mzinga wa kati wa Kitanzania) ni kama ifuatavyo:

- Urefu: mm 890
- (a) urefu wa mchi mm 482
- Upana: mm 467
- (b) Upana wa mchi mm 32
- Kimo: mm 250
- (c) Unene wa mchi mm 22
- “Lug” mm 22 x mm 12

Mchi unaweza kutumika kwenye mzinga aina ya TTBH.



Mchoro: Mzinga wa mchi (Mzinga wa kati) wa Tanzania unaoonesha sanduku na michi mivili

- Urefu: mm 890 (a) urefu wa mchi mm 482
- Upana: mm 467 (b) Upana wa mchi mm 32
- Kimo: mm 250 (c) Unene wa mchi mm 22



TTBH (wenye pande zilizoinama au mshazari)



**MIZINGA YA NYUKI KWA UENDELEU
THABITI WA UFUGAJI NYUKI NA
UHIFADHI WA MAKAZI YA TEMBO
Kata ya DOMA, KILANGALI NA
PARAKUYO
WILAYA YA KILOSA NA MVOMERO**



**Imeandaliwa na
CONASU – Morogoro**

**Kwa ufadhili wa
The Rufford Foundation (RSG)**

2016

Mizinga

Mizinga ya nyuki ni nyumba au makazi ya nyuki ya asili (matundu ya miti na mapango) au yaliyotengenezwa. Matumizi ya mizinga ni moja katika hatua muhimu za usimamizi na maendeleo katika kusimamia shughuli za ufugaji nyuki.

Ili kuhifadhi mazingira inashauriwa wafugaji nyuki watengeneze mizinga sahihi na ya gharama nafuu itakayokidhi mahitaji yao bila kuharibu mazingira. Mahitaji hayo ni kuwa na mizinga mikubwa itakayowapatia mazao mengi zaidi. Mizinga huwekwa mahali ambapo wafugaji nyuki wanapataka wenyewe kulingana na taratibu za ufugaji nyuki na mpangilio wa matumizi endelevu ya ardhi kwenye eneo husika.



Aina za mizinga

Kuna aina kuu mbili za mizinga ya kisasa



Tanzania Top Bar Hive (TTBH) yenye pande zilizosimama na inatumia viunzi 28;

Tanzania Transitional Bee Hive. una viunzi 28 na mfuniko wa kutumbukiza ili kufunika sanduku la chini yake;

Mzinga wa biashara wa Kitanzania. una masanduku mawili yanayolingana kila sanduku likiwa na viunzi 13



Utengenezaji wa mzinga wa biashara wa Tanzania hutofautiani sana na ule wa mzinga wa kati wa Tanzania. Tofauti inakuwa tu kwenye vipimo. Mbao zinazotumika ni za unene na upana uleule (Angalia kielelezo) Mzinga huu hubeba viunzi 13 na mchi wa juu wa kiunzi ni wa urefu ule ule inchi 19. Ukubwa wa mzinga huo hubadilika kwa kuongeza sanduku moja juu ya lingine.

Sanduku la chini huwa ni la kukuzia nyuki wadogo na ndimo mnamoishi malikia. Sanduku lolote linalowekwa juu ya sanduku la kukuzia nyuki wadogo huwa ni la kuhifadhi asali

Juu ya sanduku la kukuzia nyuki wadogo, huwekwa chombo kinachoitwa kitenga malikia ili kumzuia malikia asitage mayai au kukuzia nyuki wadogo humo. Kwa sababu masanduku ya mzinga huu ni madogo, mfuniko wake huwa ni mmoja tu hautenganishwi.

HIVE CONFIGURATION

